

CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE



MAHAFALI YA KUMI NA TANO (15) KAMPASI YA KIVUKONI NA MAHAFALI YA TANO (5) KAMPASI YA KARUME -ZANZIBAR 2020

Mkuu wa Chuo anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2019/2020 kwamba **Mahafali ya Kumi na Tano** yatafanyika kwenye Kampasi ya Kivukoni, **Ijumaa tarehe 27 Novemba, 2020** kuanzia **saa 4:00** asubuhi na **Mahafali ya Tano** katika Kampasi ya Karume Zanzibar yatafanyika **Jumatatu tarehe 30 Novemba, 2020** kuanzia **saa 4:00** asubuhi.

Wahitimu wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuchukua Majoho kwenye Ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru **Kampasi ya Kivukoni** kuanzia **Jumatatu, tarehe 23** hadi **Alhamisi, tarehe 26 Novemba, 2020** wakati wa saa za kazi, na kwa **Kampasi ya Karume- Zanzibar** wafike Ofisi ya PMU kuanzia **Jumatatu tarehe 23** hadi **Ijumaa tarehe 27 Novemba, 2020** kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri. **Majoho hayatatolewa siku ya Mahafali.**
 2. Kila mhitimu anatakiwa kulipa **shilingi 40,000/=** kwa ajili ya kukodi joho na fedha hizo **hazitarejeshwa**. Wanafunzi wote watatakiwa kufuata utaratibu wa malipo ya serikali ambayo ni kwa kutumia **“CONTROL NUMBER”**
 3. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 8 Disemba, 2020** kwa **Kampasi ya Kivukoni na Kampasi ya Karume- Zanzibar**. Vinginevyo **faini ya shilingi 10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho.
 4. Zoezi la namna ya kupokea vyeti (**rehearsal**) litafanyika **Alhamis, tarehe 26 Novemba, 2020** kuanzia **saa 6.00 mchana** katika uwanja wa Mahafali **Kampasi ya Kivukoni na Kampasi ya Zanzibar** zoezi hilo litafanyika **Jumapili tarehe 29 Disemba, 2020** kuanzia **saa 4:00 asubuhi** katika uwanja wa mahafali. **Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo, hataruhusiwa kushiriki katika Mahafali hayo.**
 5. Kila mhitimu atapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.
 6. Kusanyiko la wahitimu wote (**Convocation**) waliosoma katika chuo cha kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere litafanyika **Alhamis, tarehe 26 Novemba 2020** katika jengo la Utamaduni kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa sita mchana
 7. Washiriki wote wa Mahafali wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao katika Ofisi ya Mitihani kabla ya **tarehe 25 Novemba, kwa kupiga simu namba 0659120900 AU 0767245451.**
- SIMU HIZO ZIPIGWE MUDA WA KAZI TU.**

NYOTE MNAKARIBISHWA.

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
S.L.P. 9193,

DAR ES SALAAM.

Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047

Faksi: +255 22 2820816

Barua pepe: rector@mnma.ac.tz